Mfululizo wa Masuala ya Kifikihi

al-Iftaar fi ‘s-Safar

‘Alaa Dhaw’i ‘l-Kitaab wa ‘s-Sunnah

KUFUNGUA SAFARINI

KWA MUJIBU WA KITABU NA SUNNA

Kimeandikwa na:
Sheikh Jafar Subhani

Kimetarjumiwa na:
Hemedi Lubumba Selemani

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 9987 - 427 - 47 - 2

Kimeandikwa na:
Sheikh: Jafar Subhani

Kimetarjumiwa na:
Hemedi Lubumba Selemani

Kimehaririwa na:
Ustadh Abdallah Mohamed

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Ukhti Pili Rajab

Toleo la kwanza: Februari, 2008
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Al -Itrah Foundation
P. O. Box 19701, Dar-es-Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Fax: +255 22 2127555
Email: alitrah@raha.com
Website: www.alitrah.org
Online: www.alitrah.info

YALIYOMO

Kufungua Safarini kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.....2

Kufungua Safarini.....4

Kitabu na Saumu ya Ramadhani Safarini.....6

Mzima mwenye Afya.....8

Tatu: Walichofaradhishiwa hao wawili tangu mwanzo wa amri ni kufunga siku nyingine.....10

Kauli za baadhi ya wafasiri zinaupa nguvu msimamo wetu.....11

Kukisia kitenzi ‘akafungua’ ili kuoanisha Aya na madhehebu.....13

Nne: Kutaja mgonjwa na msafiri katika kifungu kimoja cha maneno.....18

Mwenye kuweza kwa mashaka.....18

Kufunga Saumu ya Ramadhani Safarini kwa mujibu wa Sunna.....23

Vigezo walivyochukua ili kuruhusu saumu Safarini.....29

Neno la mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la: "" Sisi tumekiita: "Kufungua safarini."

Kitabu hiki, "Kufungua safarini" ni matokea ya utafiti wa kielimu uliofanywa na Mwanachuoni wa Kiislamu, Sheikh Jafar Subhany.

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake.

Wanachouni wa Kiislamu kama kawaida ya wanadamu wamehitilafiana katika hukumu ndogo ndogo katika matendo ya ibada, lakini kama ilivyo, tofauti ndogo kati ya wanachuo kwa wafuasi inakuwa ni mlima wa tofauti na kusababisha zongo lisilo na maana. Mambo ambayo wanachuo wetu wamehitilafiana si katika asili au misingi ya dini, na isitoshe ni mambo machache sana ukilinganisha na yale tunayokubaliana nayo.

Kufungua safarini ni suala ambalo wanachuo wetu wamehitalifiana; ndani ya madhehebu moja na kati ya madhehebu. Kwa hiyo hii sio hitilafu ya madhehebu, bali ni hitilafi ya wanachuo wa madhehebu zote wamehitilafiana juu ya suala hili. Lakini bahati mbaya Waislamu wengi hawaitambui hitilafu hii kwa usahihi na hivyo kuongelea katika dhana na kusababisha mizozo isiyokuwa na maana. Kutokana na hali hii Sheikh wetu, Jafar Subhani amelifanyia utafiti wa kina suala hili na kuweka wazi asaili ya hitilafu hii, kisha akamuachia msomaji mwenyewe kutoa uamuzi.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya 'Al-Itrah Foundation' imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Hemedi Lubumba Selemani (Lipumba) kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 19701
Dar-es-Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 2110640

KUFUNGUA SAFARINI

KWA MUJIBU WA KITABU NA SUNNA

UTANGULIZI

Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu Mlezi wa ulimwengu. Rehma na Amani zimfikie mbora wa viumbe na hitimisho la mitume wake, pia kizazi chake kitakatifu ambacho ndio kasha la elimu yake na hazina ya mafunzo yake.

Hakika Uislamu ni imani na sheria. Imani ni kuamini Mwenyezi Mungu, mitume Wake na Siku ya Mwisho. Na sheria ni hukmu za Mwenyezi Mungu ambazo zina jukumu la kumpa mwanadamu maisha bora na kumuhakikishia wema wa dunia na akhera.

Sheria ya kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake, hivyo Mwenyezi Mungu akasema:

ٱلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ

ٱلْإِسْلَٰمَ دِينًا ۚ

“Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema Yangu na nimewapendeleeni Uislamu uwe dini yenu.” (***al-Maida;* 5:3**).

Isipokuwa kuna masuala madogo madogo ambayo wanavyuoni wa sheria wametofautiana kwa sababu ya kutofautiana kwao kuhusu

riwaya ambazo zimenasibishwa kwa Mtume, jambo lililosababisha kutofautiana kuhusu masuala madodo madogo ya sheria.

Kwa kuwa ukweli hutokana na utafiti basi hakika katika mtiririko wa masomo haya tumejaribu kuliweka swala hili juu ya meza ya utafiti, kwani huenda ikawa ndio njia ya kuunganisha mtazamo na kusogeza hatua katika uwanja huu, kwani tofauti iliyopo si katika asili na misingi ya dini hata ipelekee kuwa na uadui na chuki, bali tofauti iliyopo ni kuhusu riwaya zilizonasibishwa na Mtume, nalo ni jambo dogo ukilinganisha na mambo mengi ambayo tunaafikiana kati ya madhehebu za kiislamu.

Na muongozo wetu katika njia hii ni kauli ya Mwenyezi Mungu:

وَٱعْتَصِمُواْ بِحَبْلِ ٱللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُواْ ۚ وَٱذْكُرُواْ نِعْمَتَ ٱللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنتُمْ أَعْدَآءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُم بِنِعْمَتِهِۦٓ إِخْوَٰنًا ﴿١٠٣﴾

“Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, mlipokuwa maadui na akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema Zake mkawa ndugu.” (3:10 3).

Jafar Subhany

Taasisi ya Imamu Sadiq (a.s.)
Qum

KUFUNGUA SAFARINI

Kwa kufuata Qur'ani na Sunna mutawatiri wanavyuoni wameafikiana kuwa ni ruhusa kisheria kufungua safarini kwa hiyari au kwa wajibu, isipokuwa wametofautiana juu ya ulazima na ruhusa ya hiyari. Hii ni kama tofauti iliyopo kuhusu kupunguza; je, ni ruhusa ya hiyari au ni lazima.

Imamiya kwa kuwafuata Maimamu wa Ahlul-bait, wao na Dhahiriya wamesema kuwa kufungua ni lazima. Na katika maswahaba ndio kauli ya Abdur-Rahmani bin Aufi, Umar na mwanae Abdallah, Abu Huraira, Aisha na Ibnu Abbas.

Na kwa waliokuja baada ya maswahaba ndio kauli ya Ali bin Huseini bin Ali bin Abu Talib na mwanae Muhammad Al-Baqir, Saidi bin Al-Musayyibu, Atau, Ur'watu bin Az-Zubairi, Shaabatu, Az-Zahriy, Al-Qasim bin Muhammad bin Abu Bakar na Yunus bin Ubaydu na wafuasi wake. **1**

Wanavyuoni wa Fiq'hi wa kisunni wakiwemo wanavyuoni wa madhehebu manne wamesema kuwa kufungua ni ruhusa ya hiyari, japokuwa wametofautiana kuhusu ni kipi bora kufungua au kufunga.

Al-Jasasu amesema: "Swaumu safarini ni bora kuliko kufungua."

Malik na At-Thauriy wamesema: "Kufunga kunapendeza sana kwetu kwa mwenye nguvu ya kufunga."

Shafi amesema: "Akifunga safarini inatosheleza." **2**

1. Al-Mahaliy ya Ibnu Hazmi: 6:258
2. Ahkamul-Qur'an: 1/215

As-Sar'khasiyyu amesema: "Hakika kufunga safarini inaruhusiwa kwa kauli ya wanavyuoni wa fiq'hi, na hii ndio kauli ya maswahaba wengi, na kwa mujibu wa kauli ya watu wa dhahiri hairuhusiwi - mpaka akasema: "Hakika kufunga safarini ni bora kwetu kuliko kufungua."

Shafi amesema: "Kufungua ni bora kwa sababu dhahiri ya Hadithi tulizozipokea zinaonyesha kuwa kufunga safarini hairuhusiwi, hivyo hata kama dhahiri hii ikiachwa iruhusu funga basi itabakia kuwa kufungua ni bora."

Akalinganisha na Swala, hakika kupunguza na kuishia rakaa mbili safarini ni bora kuliko kutimiza, na hivyo ndivyo swaumu ilivyo kwa sababu safari inazibadili.

Mtume amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu alimuondolea msafiri nusu ya Swala na funga." **3**

Ibnu Al-Qadamati Al-Muqaddasiy amesema: "Hukmu ya msafiri ni hukmu ya mgonjwa anaruhusiwa kufungua na ni karaha kwake kufunga japokuwa akifunga inatosheleza. Ruhusa ya kufungua imethibiti kwa maelezo ya (Hadithi au Aya) na ij'mai na wanavyuoni wengi wamasema kuwa iwapo akifunga inatosheleza - mpaka akasema: "Kufungua safarini ni bora."**4**

Al-Qurtubiy amesema: "Wanavyuoni wametofautiana kuhusu ubora, ni kipi bora safarini, kufunga au kufungua. Malik na Shafi katika baadhi yaliyopokewa toka kwao wamesema: 'Swaumu ni bora kwa mwenye nguvu ya kufunga. Madhehebu ya Malik na ya Shafi yamefanya kuwa ni hiyari, akasema Shafi na waliomfuata kuwa: Ni

3. Al-Mabsutu ya Sar'khasiy:3/91-92

4. As-Sharhu Al-Kabiru fi dhaylul-Mughuniyi: 3/17-19

hiyari. Na wala hajaboresha, pia ndivyo ilivyo kwa Ibnu Aliyatu." **5** Nukuu hizi na nyinginezo zinaweka wazi makubaliano ya wanavyuoni wote wa fiq'hi kuwa inaruhusiwa kufungua safarini na si ulazima wa kufungua japokuwa Shafi kakiri kuwa dhahiri ya dalili ni kuzuwia kufunga safarini akasema:

Kwa sababu dhahiri ya hadithi tulizozipokea zinaonyesha kuwa kufunga safarini hairuhusiwi. **6**

Japokuwa aliyonukuu Al-Qur-tubiy na wengine toka kwake yanapingana naye.

Vyovyote vile ni kuwa kufungua ni kati ya hukmu za safari sawa iwe lazima au ruhusa ya hiyari. Muhimu ni kubainisha dalili zinazoonyesha kuwa kufungua ni lazima au ni ruhusa ya hiyari. Na itakubainikia kuwa kufungua ni lazima inayoonyeshwa na Kitabu na sunna.

Kitabu na Saumu ya Ramadhani safarini

Mwenyezi Mungu amesema: **"Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga Saumu, kama walivyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu." 7**Siku maalum za kuhesabika. Na ambaye alikuwa katika nyinyi ni mgonjwa au yuko safarini basi yampasa alipe idadi yake katika siku nyingine. Na wale waiwezayo kwa mashaka yawapasa fidia kumlisha masikini. Na ambaye atafanya kheri, basi ni kheri yake mwenyewe na mkifunga ni kheri kwenu, ikiwa mnajua. **8**

5. Al-Jamiu liahkamil'Qur'an: 2/280
6. Al-Mabsutu: 3/91
7. Al-Baqara:183
8. Al-Baqara:184

Ni mwezi wa Ramadhani iliyoteremshiwa Qur'an kuwa muongozo kwa watu, na dalili zilizo wazi za muongozo na upambanuzi. Basi mwenye kushuhudia mwezi huu na aufunge, na ambaye alikuwa mgonjwa au yuko safarini basi itampasa idadi katika siku nyingine. Mwenyezi Mungu huwatakieni yaliyo mepesi wala hawatakieni yaliyo mazito, na mtimize hesabu na kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kuwa amewaongozeni na ili mpate kushukuru." **9**

Hakika Aya hizi tukufu zimebeba hukmu za makundi manne baada ya kuwa zimehimiza kuwa Saumu ni kati ya mambo yaliyolazimishwa kwa waumini kama ilivyolazimishwa kwa wale wa kabla yao.

Mara nyingi tamko kulazimishwa ni alama ya kufaradhishwa na kuwajibishwa, na wala mukallafu haruhusiwi kuacha, hivyo Mwenyezi Mungu anawaambia waumini wote: "Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga Saumu, kama walivyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu." **10**

Hivyo Saumu imelazimishwa kwa mwanadamu kwa namna tofauti bila kutofautisha kati ya mzima mwenye afya, mgonjwa, msafiri na mwenye kuweza kwa mashaka. Lakini utekelezaji wake unatofautiana kulingana na kila hali ya mukallafu, kwa sababu kulingana na hali ni kuwa mukallafu amegawanyika katika makundi manne na kila kundi lina hukmu yake.

Mwanachuoni bora wa sheria ni yule anayepokea ufahamu wa Qur'an na Sunna, sawa iwe ufahamu huo unaafikiana na madhehebu ya imamu wake anaemfuata au unatofautiana nae.

9. Al-Baqara:185
10. Al-Baqara:184

Isipokuwa wafasiri wengi katika kutafsiri Aya hizi wamejaribu kuzioanisha na madhehebu ya maimamu wao bila ya kuzamisha mtazamo ndani ya misamiati ya aya na sentensi zake ili watoe matokeo ya aina moja bila kutofautiana.
Na bila shaka umeshajua kauli zao.

Hivyo tunasema:
Aya zilizotangulia zinabainisha hukmu ya makundi manne ambayo tayari umeshajua anuani zake. Hivyo kifuatacho ni upembuzi kuhusu kinachopatikana ndani ya aya hizi kuhusu haki za makundi haya.

Mzima mwenye Afya

Hakika kauli ya Mwenyezi Mungu: “Basi mwenye kushuhudia mwezi huu na aufunge.” inabainisha wazi ulazima wa kufunga Saumu kwa mwenye kuushuhudia mwezi, bila kutofautisha tafsiri ya kushuhudia mwezi, kati ya kuwemo ndani ya mji wa makazi bila safari au kuona mwezi muandamo. Mwenye kushuhudia hana jukumu isipokuwa moja tu nalo ni kufunga mwezi mzima iwapo tu atatimiza sharti zote.

2- Mgonjwa

Msafiri

Hakika Mwenyezi Mungu amebainisha hukmu ya mgonjwa na msafiri katika sehemu mbili:

“Na ambaye alikuwa katika nyinyi ni mgonjwa au yuko safarini basi yampasa idadi yake katika siku nyingine.” **11**

11. Al-Baqara:185

“Na ambaye alikuwa mgonjwa au yuko safarini basi itampasa idadi katika siku nyingine” **12**

Na makusudio ni kufahamu hukmu ya jukumu la mgonjwa na msafiri ndani ya sentensi katika sehemu hizo mbili. Je ni maana dhahiri inaonyesha kuwa kufungua ni lazima au ni ruhusa ya hiyari.

Na kuzama ndani ya Aya kunathibitisha kuwa kufungua ni lazima, hilo ni kwa vigezo vinne:

Kwanza: Kuwepo wajibu wa kufunga katika siku nyingine ni alama ya ulazima wa kufungua.

Hakika maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu:“Basi itampasa idadi katika siku nyingine” maana yake ni “Ni wajibu juu yake Saumu katika siku nyingine” au “Inamlazimikia Saumu katika siku hizo.”

Hili ndilo linaloonekana toka kwa wafasiri wengi kwani baada ya sentensi ‘Basi itampasa idadi katika siku nyingine’ wanasema: ‘Ni wajibu juu yake Saumu siku nyingine.’ Hivyo maana inayojulikana haraka toka kwenye Aya ni kuwa analazimikiwa kufunga katika siku hizo nyingine, au ana dhima ya kufunga. Huu ni upande mmoja.

Upande mwingine ni kuwa ikiwajibika kufunga siku hizo nyingine bila sharti lolote basi inakuwa kufungua ndani ya mwezi wa Ramadhani ni wajibu. Kwa sababu laiti ingekuwa ni ruhusa ya hiyari kufunga basi isingekuwa ni wajibu kufunga siku hizo nyingine bila kuwekwa sharti lolote. Hivyo wajibu huo wa kufunga nao pia ni alama ya wajibu wa kufungua katika mwezi wa Ramadhani.

Pili: Mukabala kati ya sentensi mbili ni dalili ya uharamu wa kufunga.

12. Al-Wasailu:7, hadithi ya 8, mlango wa 1 mlango wa anayepaswa kufunga.

Ni wazi kuwa ikiwa ndani ya maneno kuna sentensi mbili zilizo mukabala basi hali ya kutojulikana maana ya moja kati ya sentensi mbili huondoka kwa kujulikana maana dhahiri ya sentensi nyingine. Kutokana na hayo tunaondoa hali ya kutojulikana maana ya kauli 'Au yuko safarini' kwa kutumia sentensi nyingine mukabala, hivyo tunasema:
Mwenyezi Mungu kasema kuhusu atakayeshuhudia mwezi kuwa: "Basi mwenye kushuhudia mwezi huu na aufunge."

Kisha akasema kuhusu yule asiyeushuhudia mwezi: "Na ambaye alikuwa …….au yuko safarini basi yampasa idadi yake katika siku nyingine."

Hivyo ikiwa maana ya sentensi ya kwanza ni kuwa mwenye kushuhudia afunge basi kwa mujibu wa hukmu ya mukabala itakuwa maana ya sentensi ya pili ni kuwa msafiri hafungi. Hivyo kama amri ya kutenda iliyopo sentensi ya kwanza inaonyesha wajibu basi amri ya kukataza iliyopo sentensi ya pili itakuwa inaonyesha uharamu.

Imepokewa toka kwa Ubaydu bin Zarara toka kwa Imam Sadiq (a.s.) kwamba amesema: "Nilimwambia: 'Basi mwenye kushuhudia mwezi huu na aufunge'. Akasema: 'Ni hili ninalolibainisha: Mwenye kushuhudia mwezi afunge na atakayesafiri asifunge'". **13**

Tatu: Walichofaradhishiwa hao wawili tangu mwanzo wa amri ni kufunga siku nyingine

Hakika maana inayoonekana katika kauli ya Mwenyezi Mungu: "Na ambaye alikuwa katika nyinyi ni mgonjwa au yuko safarini basi yampasa idadi yake katika siku nyingine." Ni kuwa kilichofaradhishwa juu ya makundi mawili tangu mwanzo wa amri ni Saumu

13. Tafsiri Tabariy:2/77

katika siku nyingine.

Kwani ikiwa Saumu ni wajibu kwa mukallafina wote na ikawa kilichofaradhishwa kwa mukalafina wote ni Saumu katika siku nyingine (zisizo za Ramadhani) basi Saumu yao ndani ya mwezi wa Ramadhani itakuwa ni bidaa na haramu kisheria, kwani umma wote umekubaliana juu ya kutokuwepo wajibu wa Saumu mbili (moja ndani ya Ramadhani na nyingine nje ya Ramadhani) muda wote wa mwaka mzima.

Kauli za baadhi ya wafasiri zinaupa nguvu msimamo wetu

Baadhi ya wafasiri pindi wanapofasiri Aya hii tafsiri ya neno kwa neno, wamefasiri hii kwa maana tuliyoitaja, na pindi walipofika sehemu ya kubainisha je hukmu ya kufungua ni lazima au ni ruhusa ya hiyari? Fat'wa za maimamu wao ziliwazuia kudhihirisha ukweli.

At-Tabariy amesema: "Atakayekuwa mgonjwa miongoni mwenu kati ya wale waliopewa jukumu la kufunga, au mzima mwenye afya na akawa safarini basi yampasa idadi yake katika siku nyingine."

(Amesema): Ni wajibu juu yake kufunga idadi ya siku alizofungulia wakati wa ugonjwa wake au safarini, azifunge siku nyingine, yaani siku nyingine zisizo siku za ugonjwa wake au safari yake. **14**

Hivyo dhahiri ya kauli yake: Ni wajibu juu yake; kufunga idadi ya siku, ina maanisha wanalazimikiwa wao wawili kufunga idadi hiyo. Hivyo itakuwaje iwe hiyari kwao kati ya kufungulia au kufunga ilihali kuna ulazima wa kulipa uliyowekwa bila sharti lolote.

14.Tafsiril-Qur'ani Al-Adhimu: 1/376

Ibnu Kathir amesema: “Na ambaye alikuwa katika nyinyi ni mgonjwa au yuko safarini basi yampasa idadi yake katika siku nyingine” Yaani mgonjwa na msafiri wao wawili hawafungi katika hali yao ya ugonjwa na safari kutokana na uzito juu yao, bali wanafungua na watalipa idadi hiyo katika siku nyingine. **15**

Wakati huo huo baada ya ukurasa huo amesema: “Basi mwenye kushuhudia mwezi huu na aufunge.” Hivyo Mwenyezi Mungu amethibitisha funga yake kwa mkazi asiye safarini na ametoa ruhusa ya hiyari kwa mgonjwa na msafiri. **16**

Hebu tazama iko wapi kauli yake “Wao wawili hawafungi katika hali yao ya ugonjwa na safari,” mbele ya kauli yake “Na ametoa ruhusa ya hiyari kwa mgonjwa na msafiri.”

Maelezo ya mwanzo ni maelezo yaliyotokana na maana ionekanayo kwenye aya, ambayo imepita kwenye kalamu yake bila kujijua bila kutizama madhehebu ya imamu wake. Na maelezo ya pili yamemtoka kwa lengo la kuipa nguvu rai ya imamu wa madhehebu yake.

15. Tafsiril-Qur’ani Al-Adhimu: 1/376

16. Rejea iliyotangulia:1/378

Kukisia kitenzi ‘akafungua’ ili kuoanisha Aya na madhehebu

Kisha baadhi ya wafasiri walipojua kuwa maana inayoonekana kwenye Aya ni ulazima wa kufungua na kufunga siku nyingine ikiwa ni sehemu ya siku zile alizofungua, wamejaribu kuoanisha Aya na madhehebu yanayotoa ruhusa ya hiyari, hivyo wakakisia kuwepo tamko “kisha akafungua.”

Wakasema: “Kisha akafungua basi yampasa idadi yake katika siku nyingine. Hivyo ni kama vile na wao wamewajibikiwa na Saumu ndani ya mwezi wa Ramadhani lakini wana hiyari. Hivyo iwapo wakifungua basi ni wajibu juu yao kufunga idadi hiyo, na iwapo hawakufungua basi si wajibu.

Tafsiri hii haina malengo mengine isipokuwa ni kuoanisha aya na madhehebu bila kutafsiri aya kama ilivyo. Na hapa tunakuletea baadhi ya mifano ya maneno yao:

Hakika Imamu Ar-Raziy ni miongoni mwa watu waliotoa dalili ya anaesema kuwa kufungua ni lazima wala si ruhusa ya hiyari, lakini pamoja na hayo akachagua msimamo mwingine kwa hoja ya kuwa katika aya kuna kisio, yaani “kisha akafungua” au ulazima wa kulipa unatokana na kufungua makusudi si kwa ugonjwa na safari. Amesema: “Kundi la wanavyuoni wa maswahaba wameona kuwa ni lazima kwa mgonjwa na msafiri kufungua na aje afunge idadi hiyo siku nyingine, na hiyo ndio kauli ya Ibnu Abbas na Ibnu Umar.

> Wanavyuoni wengi wa fiq’hi wameona kuwa kufungua ni ruhusa ya hiyari, hivyo akitaka afunge asipotaka afungue. Kuthibitisha

hilo wanavyuoni wametoa hoja zifuatazo:

KWANZA: Hakika ndani ya aya kuna mficho wa neno. Nalo hukisiwa ni: Kisha akafungua basi yampasa idadi yake katika siku nyingine.

PILI: Aliyoyataja Al-Wahidiy ndani ya kitabu *Al-Basitu* amesema: 'Ulazima wa kulipa unatokana na kufungua makusudi si kwa ugonjwa na safari.'

TATU: Aliyoyapokea Ibnu Daud katika Sunan yake toka kwa Hisham…….Hakika Hamza Al-Aslamiy alimuuliza Mtume akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, je nifunge safarini? Akasema: Ukitaka funga na ukitaka fungua." **17**

Hoja ya kwanza inajibiwa kuwa: Mficho wa neno ni kinyume na maana inayoonekana. Na wala hakuna dalili yoyote juu ya kisio hilo isipokuwa ni kuoanisha Aya na madhehebu ya kifiq'hi.

Hoja ya pili inajibiwa kuwa: Ni dai lisilo na dalili yoyote. Maana inayoonekana kwenye aya na riwaya ambazo zitakufikia mbele vyote vinaonyesha kuwa safari haikusanyiki na Saumu pamoja, hiyo ni sawa afungue au asifungue.

Ama hoja ya tatu ni kuwa subiria baadaye utaona hali ya riwaya ilivyo.

Katika juhudi za kuoanisha Aya na fat'wa ya madhehebu ya wanavyuoni wa fiq'hi ya kisunni, mwandishi wa *Al-Manar* amesema: "Na ambaye alikuwa katika nyinyi ni mgonjwa au yuko safarini basi yampasa idadi yake katika siku nyingine" Yaani ambaye alikuwa hivyo "kisha akafungua" ni wajibu juu yake kufunga idadi

17. At-Tafsirul-Kabir: 5/74 na 76

hiyo siku nyingine zisizokuwa siku maalumu za kuhesabika. Hivyo iwapo atafungua basi wajibu juu yake ni kulipa kulingana na idadi ya siku ambazo hajafunga. **18**

Nasema: Kilichompelekea mfasiri wa *Al-Manar* kukisia kauli "Kisha akafungua" au kauli "Iwapo akifungua" ni baada ya kukuta aya inaonyesha ulazima wa kufungua na kuwa wajibu juu yake ni kufunga idadi hiyo siku nyingine, hivyo akajaribu kukisia uwepo wa "Iwapo akifungua" ili aiondoe aya kwenye maana yake inayoonekana wazi na aifanye ionyeshe hiyari kati ya kufunga Ramadhani na kufunga idadi katika siku nyingine.

Na la kushangaza ni kuwa katika sehemu nyingine ya maneno yake ametamka wazi kuwa ni "mbeuo" hapo maneno yake yanamaanisha kuwa ameiondoa Aya kwenye maana yake inayoonekana bila kuwepo dalili yoyote (inayoruhusu hilo).

Amesema: "Waliotutangulia wametofautiana kuhusu suala hili, hivyo kundi moja likasema: 'Saumu haitoshelezi faradhi, bali atakayefunga safarini ni wajibu juu yake kulipa asipokuwa safarini, hiyo ni kutokana na maana inayoonekana katika kauli: "Basi itampasa idadi katika siku nyingine" ……Maana ionekanayo ni wajibu juu yake idadi, au ni wajibu idadi. Wanavyuoni wa fiq'hi ya kisunni wakaibeua kwa kudai kuwa kisio ni: Kisha akafungua basi itampasa idadi." **19**

Wala siachi kumshangaa kwani anasema kuwa ni mbeuo, lakini pamoja na hilo anang'ang'ania kudai kuwa fat'wa ya wanavyuoni wa fiq'hi ni Sahihi, huku mwanzo wa tafsiri yake amewaumbua wale wanaofuata maimamu wa madhehebu yao ilihali wakibeua maana dhahiri ya aya ili kuoanisha na fat'wa za madhehebu za maimamu

18. Tafsiril-Manari: 2/150

19.Tafsiril-Manari: 2/153

wao.

Katika suala la talaka tatu amesema: "Kusudio si kuwajadili wanaofuata au kuwatoa makadhi na mamufti toka kwenye madhehebu yao, kwani wengi wao wanazikuta Hadithi hizi ndani ya vitabu vya Hadithi na vinginevyo na wala hawazijali. Kwa sababu matendo kwao ni kutokana na kauli za vitabu vyao na wala si kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume Wake. **20**

Wanavyuoni wengi wa Shia Imamiyya wamemjibu yule anayekisia "Kisha akafungukia" kwa lengo la kutaka kuthibitisha ruhusa ya hiyari.

Sheikh Tusi amesema: "Na katika Aya hii kuna dalili inayothibitisha kuwa msafiri na mgonjwa ni wajibu juu yao kufungua, kwa sababu Mwenyezi Mungu amewawajibisha kulipa bila kuweka sharti lolote, na kila aliyewajibishwa kulipa kutokana na safari na ugonjwa amewajibishwa kufungua……"

Hivyo wakikisia "Kisha akafungua" katika Aya itakuwa ni kwenda kinyume na aya. Na kati ya waliosema ni wajibu kufungua safarini ni Umar bin Al-Khattab. (Ametaja majina ya maswahaba na waliokuja baada ya maswahaba ambao tulitaja majina yao mwanzo wa uchambuzi wa mada hii, wote wakisema ni wajibu kufungua." **21**

Mwanachuoni Tabatabai amesema: "Na ambaye alikuwa katika nyinyi ni mgonjwa au yuko safarini basi yampasa idadi yake katika siku nyingine" (*Fau)* hapo ni ya kuzalisha sentensi, na hapo sentensi imetokana na "Mmelazimishwa."

20. *Tafsiril-Manari*: 2/386

21. *At-Tibyani:* 2/150

Na kauli: “maalumu za kuhesabika” maana yake ni kuwa Saumu waliyolazimishwa imefaradhishwa juu yao waifunge ndani ya siku hizo.

Kisha akasema: “Wenye kusema ni ruhusa ya hiyari wamekisia, wakasema: Hakika kisio ni: Na ambaye alikuwa katika ninyi mgonjwa au yuko safarini kisha akafungua basi yampasa idadi yake katika siku nyingine.

Wanajibiwa kuwa kwanza: Hakika kisio ni kwenda kinyume na maana dhahiri ionekanayo katika aya na huwa haikubaliki kukisia isipokuwa mpaka kuwe na alama, na katika maneno hayo hakuna alama yoyote juu ya kisio hilo.

Pili: Hata kama tukikubali kuwepo kisio bado maneno yatakuwa hayaonyeshi ruhusa ya hiyari, kwani muda huo kama walivyosema ni kipindi cha kuweka sheria, na kinachoonyeshwa na kauli yetu: “Na ambaye alikuwa katika nyinyi ni mgonjwa au yuko safarini kisha akafungua” ni kuwa kufungua si kosa, bali ni ruhusa kwa maana pana yenye kujumuisha wajibu, sunna na ruhusa ya hiyari.

Ndani ya maneno hayo yaliyokisiwa hamna dalili yoyote juu ya dai la kuwa: Kauli hiyo inaonyesha ruhusa ya hiyari tu. Bali ndani yake kuna dalili inayothibitisha kinyume chake, kwani ni dhahiri kuwa dai la kuwa: Maneno hayajabainisha kile cha lazima kubainishwa kipindi cha kuweka sheria ni dai lisilolingana na muweka sheria mwenye busara”. **22**

22. *Al-Mizani*: 2/11

NNE: KUTAJA MGONJWA NA MSAFIRI KATIKA KIFUNGU KIMOJA CHA MANENO.

Hakika aya imemtaja mgonjwa na msafiri katika kifungu kimoja cha maneno na ikawawekea hukmu moja ikasema: “Basi yampasa idadi yake katika siku nyingine”. Hivyo je ruhusa ya hiyari ni haki ya msafiri tu, au inajumuisha msafiri na mgonjwa.

Kwanza: Inalazimisha kutenganisha, kwani maana dhahiri ya aya ni kuwa makundi yote mawili yana hukmu moja wala hayatofautiani, hivyo dai la kuwa hukmu ya kufungua linamuhusu msafiri tu bila kumgusa mgonjwa dai hilo halinasibiani na maana dhahiri ya aya.

Pili: Je, inasihi kwa mwanavyuoni wa fiq’hi kutoa fat’wa ya ruhusa ya hiyari kwa mgonjwa ikiwa Saumu inamdhuru au ni uzito kwake?!. Hakika kujidhuru ni haramu kwa mujibu wa sheria takatifu, pia kujiwekea uzito katika kutekeleza faradhi ni jambo lisilotakiwa wala lisiloruhusiwa ndani ya sheria. Mwenyezi Mungu amesema: “Wala hakuweka juu yenu uzito katika dini”. **23**

4- MWENYE KUWEZA KWA MASHAKA

Hili ndio kundi la nne ambalo Mwenyezi Mungu amebainisha hukmu yake kwa kusema: “Na wale waiwezayo kwa mashaka yawapasa fidia kumlisha masikini.”

Je makusudio hapo ni mzee na bibi kizee vikongwe ambao hawawezi kufunga au ni wasioweza kufunga ila kwa taabu sana?

23. ***Al-Hajj:*** **78**

Dhahiri ni wa pili. Kwa sababu kitenzi hiki (Itaqat) humaanisha kiwango cha chini cha uwezo na nguvu ya utendaji, hivyo waarabu hawatumii kitenzi hiki isipokuwa pale uwezo na nguvu ya utendaji utakapokuwa katika kiwango cha chini kabisa kiasi kwamba mtendaji anatenda kwa kujikaza.

Vyovyote vile itakavyokuwa ni kuwa wajibu kwake ni kutoa fidia. Wanavyuoni wametofautiana kuhusu kiwango cha fidia kama ilivyoelezwa ndani ya fiq'hi zao. Yupo aliyesema kuwa ni nusu ya pishi, na hao ni watu wa Rai. Shafiy akasema: "Kibaba kwa kila siku." Na ndio kauli ya madhehebu ya Shia Imamiyya.

Lakini kiwango hicho kinasihi isipokuwa yule mwenye uwezo wa kuongeza zaidi ya kiwango hicho basi ndio kheri. Kama anavyosema Mwenyezi Mungu: "Na ambaye atafanya kheri basi ni kheri yake mwenyewe." Yaani akalisha zaidi ya maskini mmoja basi ni kheri.

Kisha hapa kuna tafsiri mbili nyingine za mwenye kufanya kheri:

Sentensi inamhusu mwenye kuweza kwa taabu, na mwenye kheri anayekusudiwa ni yule atakayekusanya kati ya Saumu na sadaka.

Anajibiwa kuwa: Tafsiri hiyo iko mbali na maana inayoonekana kwenye Aya. Hebu tujaalie kuwa kuna mzee kikongwe asiyeweza kufunga isipokuwa kwa kutoa juhudi na nguvu zake zote. Je ni Sunna kwake kukusanya Saumu na sadaka pamoja? Zaidi ya hapo itakuwaje mwenye uwezo wa kufunga analazimikiwa na Saumu tu peke yake, wala si Sunna kwake kutoa fidia lakini kikongwe ni Sunna kwake Saumu iliyo pamoja na fidia!!

Sentensi inawahusu wenye udhuru, yaani mgonjwa na msafiri. Makusudio hapo ni kuwa akizidisha juu ya siku hizo maalumu za kuhesabika basi ni kheri kwake, kwa sababu thawabu na faida ya

kuzidisha ni ya kwake. Hivyo "*Fau*" katika kauli: "Na ambaye atafanya kheri" hapo inaonyesha hilo. Kwa sababu sentensi hiyo ni tawi lililokuja baada ya kuwa faradhi imehusishwa ndani ya siku maalum tu zenye kuhesabika. **24**

Anajibiwa kuwa: Itakuwaje sentensi iwahusu wenye udhuru ilihali kati yao na sentensi hiyo kuna hukmu ya kundi la nne? Amesema: "Na ambaye alikuwa katika ninyi ni mgonjwa au yuko safarini basi yampasa idadi yake katika siku nyingine." "Na wale waiwezayo kwa mashaka yawapasa fidia kumlisha masikini." Na ambaye atafanya kheri basi ni kheri yake."

Dhahiri ni kuwa sentensi hiyo inarejea kwenye kundi la nne. Na sentensi hiyo ni tawi lililokuja baada ya faradhi kuhusishwa na kulisha maskini. Hivyo makusudio yake ni kuwa: Na ambaye atakayefanya kheri kwa kuzidisha kulisha masikini basi ni kheri kwake.

Mpaka hapa imetimia hukmu ya makundi manne.

* * * * *

Imebakia kuzungumzia tafsiri ya kauli: "Na mkifunga ni kheri kwenu."

Tunasema: Ni nani anayeambiwa katika kauli: "Na mkifunga ni kheri kwenu." Kisha baada ya Mwenyezi Mungu kubainisha hukmu ya makundi manne akawaambia waumini wote kwa mara nyingine: "Na mkifunga ni kheri kwenu ikiwa mnajua."

Uwambiwaji huu ni sawa na uambiwaji uliyopita, yaani kauli ya Mwenyezi Mungu:

24.*Tafsiril-Manari*: 2/158

“Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga Saumu.”

Na tofauti iliyopo kati ya maelezo hayo mawili ni kuwa maelezo ya mwanzo ni maelezo kwa ufupi na wito wa kufunga. Na maelezo ya pili ni maelezo baada ya kufafanua hukmu za makundi manne. Hivyo matokeo yake ni kuwa:
Enyi waumini ikiwa mtafunga kwa namna iliyotajwa ndani ya aya basi itakuwa kheri kwenu. Yaani anafunga mwenye kushuhudia mwezi, na anafungua mgonjwa na msafiri na atakuja kufunga siku nyingine, na mwenye kuweza kwa taabu anatoa fidia.

Ama yule anayedai kuwa ni ruhusa ya hiyari kwa msafiri na mgonjwa au kwa msafiri tu yeye anafanya maelezo hayo ni kigezo cha ruhusa ya hiyari, hivyo anasema: “Hakika maelezo hayo wanaambiwa wale wenye ruhusa ya hiyari, na kuwa kufunga ndani ya Ramadhani ni kheri kwao kuliko kutumia ruhusa kwa kufungua.”

Anajibiwa kuwa: Tafsiri hiyo inatokana na kitendo cha kutaka kujaribu kuilazimisha Aya ifuate madhehebu yake ya kifiq’hi nayo ni kuwa na hiyari ya kufunga au kufungua, lakini hata hivyo tafsiri hiyo si sahihi kwa vigezo viwili:

Hakika kugeuza maelezo wanayoambiwa watu wote kwa kuyafanya kuwa maelezo wanayoambiwa kundi maalum ni tafsiri isiyokuwa na shikio lolote la dalili, na tafsiri hiyo ni tawi la tafsiri ya rai binafsi.

Laiti kama maelezo yangekuwa ni ya wenye ruhusa ya hiyari basi ingelazimika aseme: Na msafiri akifunga ni kheri kwake kuliko kufungua, abainishe hukmu kwa dhamiri ya asiyekuwepo si kwa dhamiri ya aliyepo.

Dhahiri ni kuwa kutilia mkazo juu ya utekelezaji wa faradhi na kuwa Saumu ni kheri ni jambo lenye matunda mazuri ndani ya nafsi,

kwani kujiepusha na kitendo cha kujihimiza kukusanya ladha za kimwili na kujizuia na matamanio kunasababisha uchamungu na kujitenga na wazo la kuishi daima duniani.

Kwa ufafanuzi zaidi tunasema kuwa Aya ya pili imetokana na vipengele vinne, hiyo ni baada ya kubainisha kuwa wajibu hauzidi ndani ya siku maalum za kuhesabika:

Cha kwanza: Na ambaye alikuwa katika nyinyi ni mgonjwa au yuko safarini basi yampasa idadi yake katika siku nyingine.

Cha pili: Na wale waiwezayo kwa mashaka yawapasa fidia ya kumlisha masikini.

Cha tatu: Na ambaye atafanya kheri basi ni kheri yake mwenyewe.

Cha nne: Na mkifunga ni kheri kwenu ikiwa mnajua.

Vipengele vitatu vya mwanzo vimekuja kwa tamko la asiyekuwepo, kinyume na cha mwisho, chenyewe kimekuja kwa tamko la aliyekuwepo.

Na hii ni dalili kuwa kimejitenga na vipengele vitatu vya mwanzo na kimekuja kwa ajili ya kutilia mkazo maelezo ya mwanzo baada ya ufafanuzi, yaani kutilia mkazo kauli ya Mwenyezi Mungu: “Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga Saumu”

* * * * *

Kisha Mwenyezi Mungu katika Aya ya tatu ametaja sentensi tatu: Mwenyezi Mungu huwatakieni yaliyo mepesi wala hawatakieni yaliyo mazito.

Maelezo hayo ni kubainisha hekma ya makundi matatu kuondolewa Saumu. Yaani wamelazimishwa kufungua kwa ajili ya kupewa wepesi na kuondolewa uzito, bila ya kutofautisha kati ya mgonjwa au msafiri au anayefunga kwa mashaka.

Na mtimize hesabu.

Maelezo haya yanarejea kwenye malipo ya mgonjwa na msafiri. Yaani kilichoondolewa kwao ni Saumu ndani ya mwezi wa Ramadhani, ama kulipa kwa idadi ya siku maalum kwenyewe hakujaondolewa.

Na kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kuwa amewaongozeni na ili mpate kushukuru.

Sentensi inaonyesha lengo la asili ya Saumu kiasi kwamba Mwenyezi Mungu anawataka waja Wake kumtukuza kwa vile alivyowaongoza ili waweze kumshukuru kwa neema Yake.

Hii ni tafsiri ya Aya tatu kulingana na maana dhahiri inayoonekana kwenye ufunuo huo.

KUFUNGA SAUMU YA RAMADHANI SAFARINI KWA MUJIBU WA SUNNA

Umeshajua hukmu ya Kitabu kuhusu kufunga safarini, na kuwa wajibu ni kufungua na kuja kulipa siku nyingine kwa kadiri alivyofungua. Hebu hivi sasa twende kwenye Sunna na tusome riwaya zinazohusu hilo.

Mwisho utaelewa kuwa riwaya zinaunga mkono Qur'ani na wala

haziipingi hata kidogo. Bali sharti ni kuzama ndani ya maana na mtiririko wa wapokezi wa riwaya hizo. Ama riwaya zilizopokewa kwa njia ya Ahlul-baiti ni nyingi sana kiasi kwanba haitoshi kuzinukuu hapa, bali tutanukuu chache tu ili tupate baraka zake:

Kulayniy amepokea kwa njia yake toka kwa Az-Zahriyyu toka kwa Ali bin Huseini amesema katika hadithi: Ama Saumu ya msafiri na mgonjwa hakika masunni wametofautiana kuhusu hilo. Wengine wamesema anafunga. Kundi lingine limesema hafungi.

> Na wengine wamesema akitaka anafunga na akipenda hafungi. Ama sisi tunasema: Anafungua katika hali zote mbili, hivyo akifunga katika hali ya safari au ya ugonjwa basi ni wajibu juu yake kulipa, kwani Mwenyezi Mungu anasema: "Na ambaye alikuwa katika nyinyi ni mgonjwa au yuko safarini basi yampasa idadi yake katika siku nyingine." Hii ndio tafsiri ya Saumu. **25**

Kulayniy amepokea kwa njia yake toka kwa Zarara toka kwa Abu Jafar amesema: "Kuna watu Mtume aliwaita waasi pindi walipofunga ilihali yeye kafungua na kupunguza. Akasema: Wao ni waasi mpaka siku ya Kiyama, na hakika sisi tunawajua watoto zao na watoto wa watoto zao mpaka leo. **26**

Kulayniy amepokea toka kwa Ubaydu bin Zarara amesema: "Nilimwambia Abu Abdillah kuhusu kauli ya Mwenyezi Mungu: "Basi mwenye kushuhudia mwezi huu na aufunge." Akasema: Ni hili ninalobainisha: Atakayeushuhudia mwezi huu na aufunge na iwapo akisafiri basi na asiufunge." **27**

25. *Tafsiril-Manari*: 2/158

26. Al-Kafi: 4/83 mlango wa vigezo vya Saumu

27. Al-Kafi: 4/127 mlango wa karaha kufunga safarini, hadithi ya 6

Kulayniy amepokea toka kwa Ibnu Abi Umayri toka kwa baadhi ya wafuasi wake toka kwa Abu Abdillah amesema: "Nilimsikia akisema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa: Hakika Mwenyezi Mungu alimpa sadaka mgonjwa na msafiri wa umma huu kwa kumpa kupunguza na kufungua, hivi inamfurahisha mmoja wenu kukataliwa sadaka atakapotoa.?" **28**

Kulayniy amepokea toka kwa Aisu bin Al-Qasim toka kwa Abu Abdillah amesema: "Mtu atakapotoka kwa safari ndani ya mwezi wa Ramadhani anapasa kufungua. Akasema: Hakika Mtume alitoka Madina kuelekea Makka ndani ya mwezi wa Ramadhani akiwa na watu wakiwemo watembea kwa miguu, alipofika eneo la Kurail-ghamimi aliomba chombo chenye maji ikiwa ni kati ya adhuhuri na alasiri akanywa na akala, kisha watu wakafungua pamoja naye, na wengine wakatimiza Saumu zao, hivyo Mtume akawaita kuwa ni waasi na mwisho huchukuliwa amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu.**29**

Hizi ni baadhi ya riwaya zilizopokewa toka kwa Maimamu wa Ahlul-bait tumezitaja kama mfano tu na hizi ni chache kati ya nyingi, na inajulikana kuwa Maimamu wa Ahlul-bait ni moja ya vizito viwili alivyoviacha Mtume katika umma huu ili viulinde dhidi ya upotevu, hivyo kauli ya yoyote yule hailingani na kauli yao.

Na bahati nzuri sana ni kuwa riwaya za Masunni zinaafikiana na zile zilizopokewa toka kwa Ahlul-bait. Hivyo hapa tunazitaja baadhi kama ifuatavyo:

Mashekhe wawili ndani ya *Sahih* zao wamepokea toka kwa Jabir bin Abdillah Al-Answariy kuwa Mtume alikuwa safarini, ghafla akaona

28. Rejea iliyopita, Hadithi ya 1

29. Rejea iliyopita, Hadithi ya 2

kundi la watu ilihali kati yao kuna mtu kawekewa kivuli, akauliza: 'Vipi huyu?' Wakasema: 'Ni mwenye Saumu.' Akasema: 'Si wema kufunga safarini. Na kwa tamko la Muslimu ni: Si wema ninyi kufunga safarini." **30**

Hakika wema kwa matumizi ya Qur'an ni tendo zuri ambalo kinyume chake ni dhambi. Mwenyezi Mungu anasema: "Na msaidiane katika wema na uchamungu na wala msisaidiane katika dhambi na uadui." **31** Hivyo ikiwa kufunga safarini si wema basi ni dhambi na hukmu ya dhambi iko wazi.

Japokuwa kauli ya Mtume ilitoka kwa aliyekuwa ndani ya taabu kubwa lakini ametoa kanuni kuu ya kila mwenye kufunga safarini, sawa iwe ni taabu kwake au la. Ushahidi juu ya hilo ni kuwa laiti eneo la hukmu lingekuwa ni Saumu yenye kutaabisha basi angewajibika kuhimiza hilo na kusema kuwa si wema kufunga Saumu yenye kutaabisha au angetumia Aya ya Mwenyezi Mungu: "Wala hakuweka juu yenu uzito katika dini."

Ibnu Hazmi amesema: "Iwapo wakisema Mtume alikataza katika hali kama hiyo tu. Tunasema: Hili ni batili hairuhusiwi, kwa sababu hali kama hiyo imeharamishwa. Kwani kufikia hali kama hiyo ni kwa mtu yeye mwenyewe kuchagua kufunga sawa iwe pasipo safarini au safarini, hivyo kitendo cha Mtume kukataza kufunga safarini kwa kuhusisha safari tu ni kubatilisha dai alilozushiwa Mtume, na ni wajibu kuchukua maneno yake kwa mjumuisho. **32** (Yaani ni katika hali ya uzito na taabu, na isiyo ya uzito na taabu).

---

30. Rejea iliyopita, Hadithi ya 5. *Shar'hu Sahih Muslim* ya An-Nawawiy *Sahih Bukhari*: 3/44. *Sahih Muslim*:7/233

***31. Al-Maida*: 2**

32. Al-Mahaliy: 6/254

Muslim amepokea toka kwa Jabir bin Abdillah kuwa Mtume alitoka kuelekea Makka mwezi wa Ramadhani mwaka wa ukombozi wa Makka akafunga mpaka alipofika Kiraul-ghamimi, watu wakaendelea kufunga, kisha akaomba chombo chenye maji akakiinua mpaka watu wote wakakiona kisha akanywa. Baada ya tukio hilo wakamwambia: 'Hakika baadhi ya watu bado wamefunga' Akasema: "Hao ni waasi, hao ni waasi." **33**

Makusudio ya kuasi ni kwenda kinyume na amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Allah anasema: "Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake hakika amepotea upotovu ulio wazi. **34**

Na la kushangaza ni kuwa yule anayetaka kutetea madhehebu ya imamu wake anatafsiri Hadithi kuwa amri ilikuwa ni ya Sunna, lakini yuko mbali na ukweli kwani utalinganishaje amri ya Sunna na kauli ya Mtume ya: "Hao ni waasi, hao ni waasi."

Ibnu Majah ametoa toka kwa Abdurahmani bin Aufi amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: 'Mwenye kufunga Ramadhani safarini ni kama mwenye kufungua pasipo safari.'" **35**

Hadithi hii inaonyesha wazi kuwa kufungua ni lazima, kwani ikiwa ni dhambi na ni haramu kufungua safarini basi na kufunga kunakuwa ni dhambi, yaani kufunga ndani ya mwezi huu ni dhambi na ni haramu.

Ibnu Maja amepokea toka kwa Anas bin Malik toka kwa mtu wa Bani Abdul-ash'hali amesema: "Zilijifakharisha juu yetu ngamia za Mtume, hivyo nikaja kwa Mtume nikamkuta akila chakula.

33. Shar'hu Sahih Muslim ya An-Nawawiy: 7/232

***34 Al-Ahzab*: 36**

35. Sunan Ibnu Majah: 1/532, namba 1666. *Sunan Abi Daud* :2/217 namba 2407

Akaniambia: Karibia ule. Nikamwambia hakika nina Saumu. Akasema: Kaa nikusimulie kuhusu Saumu au kufunga, hakika Mwenyezi Mungu amemuondolea msafiri nusu ya Swala, na amewaondolea msafiri, mwenye mimba na mwenye kunyonyesha Saumu au kufunga. Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika Mtume aliyatamka maneno yote mawili au moja. Ningehuzunikia nafsi yangu kama nisingekula chakula cha Mtume." **36**

Abu Daud amepokea kuwa Dah-yatu bin Khalifa alitoka kijiji kimoja huko Damascas ndani ya Ramadhani, mwendo wa kufika kijiji cha Uqubati kwa kutokea Al-Fastatu, ikiwa ni umbali wa maili tatu, kisha akafungua na watu wengine wakafungua pamoja naye, ilihali wengine wakikataa kufungua. Aliporudi kijijini kwake akasema: "Naapa kwa Mwenyezi Mungu, hakika leo nimeona jambo ambalo sikutegemea kuliona, hakika kuna watu wamejitenga na uongofu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akiwaambia hayo wale walioendelea na Saumu, kisha akasema: Ewe Mwenyezi Mungu nichukue nije kwako."**37**

Hizi ni baadhi ya riwaya zinazotolewa kuthibitisha kuwa kufungua ni lazima, nyingine tumeziacha kwa kuwa mada hii tumeizungumzia ndani ya kitabu chetu "*Al-Bidaatu*" kwa kunukuu riwaya zilizomo ndani ya *Sahih Sita* na *Sunan*. Hivyo atakayetaka ufafanuzi zaidi arejee kitabu hicho.

36.Sunan Ibnu Majah: 1/533 namba 1667

37..Sunan Abi Daud: 2/319 hadithi namba 2413

VIGEZO WALIVYOCHUKUA ILI KURUHUSU SAUMU SAFARINI

Kuna baadhi ya riwaya wanazoshikilia kuthibitisha kuwa kufungua ni ruhusa ya hiyari na kuwa mukallafu ana hiyari ya kufungua au kufunga.

Kabla hatujazama ndani ya uchambuzi huu tunapenda kumkumbusha msomaji aweze kuangalia mambo matatu kwa makini sana na mwisho itamdhihirikia hali halisi ya riwaya hizo walizozitaja.

Hakika uchambuzi unahusu hukmu ya funga ya mwezi wa Ramadhani safarini, je kufunga ni lazima au ni ruhusa ya hiyari. Hivyo Saumu nyingine isiyo ya Ramadhani si maudhui ya uchambuzi wetu, na iko mbali na uchambuzi wetu.

Hakika Mtume aliamrisha kufungua ndani ya mwaka wa ukombozi wa Makka (Mwaka wa nane wa Hijiria) kabla ya hapo hukmu ya Saumu safarini ilikuwa ni ruhusa ya hiyari. Hivyo kama kuna Hadithi inayoonyesha ruhusa ya hiyari basi ili isihi inatakiwa iwe ni ya baada ya mwaka wa ukombozi wa Makka. Ama kinyume na hivyo itakuwa hadithi hiyo iko nje ya maudhui yetu kwani ruhusa ya kabla ya mwaka wa ukombozi si maudhui ya uchambuzi wetu.

Na iwapo tukijalia kuwa riwaya hizo zinaonyesha ruhusa ya hiyari basi kutakuwa na mgongano kati ya zile zinazoamrisha kufungua na hizo zinazoonyesha hiyari. Hivyo ni lazima turejee kwenye vigezo vya ziada, na hapo zitakazoafikiana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu ndipo zitakuwa hoja na dalili na kuwa sio zile zinazopingana na kitabu.

Hivyo baada ya haya mambo matatu, sasa tunasoma riwaya zinazo-

toa ruhusa ya hiyari. Tunasema: Hakika riwaya hizo ziko katika makundi:

a) Ambazo hazitamki wazi kuhusu mwezi wa Ramadhani.

Bukhari amepokea toka kwa Aisha kuwa Hamza bin Amru Al-Aslamiy alimwambia Mtume: 'Je nifunge safarini – Na alikuwa mwingi wa Saumu - Akasema: "Ukitaka funga ukitaka fungua." **38**

Hakika kauli yake: "Na alikuwa mwingi wa Saumu," inafaa kuwa dalili na alama ya kuwa swali lake lilikuwa kuhusu Saumu ya Sunna. Na hata kama neno hilo si alama lakini bado hadithi haitamki wazi kuwa ni Saumu ya mwezi wa Ramadhani. Na kama hali ndio hiyo basi Hadithi hiyo haiwi hoja.

Bukhari amepokea kwa njia yake toka kwa Abudar'dau kuwa amesema: "Tulitoka na Mtume katika baadhi ya safari zake, ilikuwa siku ya joto kali mpaka ilifikia mtu anaweka mikono yake juu ya kichwa chake kwa ajili ya ukali wa joto, na hakukuwa na yeyote aliyefunga isipokuwa Saumu ya Mtume na Ibnu Rawahati."**39**

Anajibiwa kwa jibu lile la riwaya iliyotangulia, nalo ni kuwa riwaya haijadhihirisha kuwa ni Saumu ya Ramadhani, hivyo nayo si hoja. Japokuwa inawezekana Saumu hii ilikuwa kabla ya mwaka wa ukombozi wa Makka.

Bukhari amepokea toka kwa Anas bin Malik amesema: "Tulikuwa tukisafiri na Mtume, na wala mwenye kufunga hakumkosoa mwenye kufungua wala mwenye kufungua hakumkosoa mwenye kufunga."**40**

Anajibiwa kuwa: Hadithi hii haitamki kuwa ni Saumu ya Ramadhani, kisha kitendo cha maswahaba kunyamaza si hoja ya

38. Sahih Bukhari: 3/43
39. Sahih Bukhari: 3/43
40. Sahih Bukhari: 3/44

kisheria, kwani baada ya utume wa Mtume (s.a.w.w.) hakuna utume mwingine mpaka iwe kunyamaza kwao ni hoja. Na pia inawezekana hilo lilitokea kabla ya mwaka wa ukombozi, na tayari umeshaona jinsi Mtume alivyowakhalifu waliofunga siku hiyo ya ukombozi na akasema: “Hao ni waasi, hao ni waasi.”

Muslim amepokea kwa njia yake toka kwa Tausi toka kwa Ibnu Abbas kuwa amesema: “Msimkosoe anayefunga wala anayefungua, kwani hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alifunga safarini na alifungua.” **41**

Hadithi hii haitamki wazi mwezi wa Ramadhani wala haionyeshi mwezi huo, japokuwa inawezekana ilikuwa ni kabla ya mwaka wa ukombozi. Na ndio hali ya riwaya alizozinukuu Muslim ndani ya *Sahih* yake **42** na alizozitaja Ibnu Hazmi ndani ya “Al-Mahaliy” toka kwa Ali. **43**

b) Zinazotamka wazi mwezi wa Ramadhani lakini hazitamki kuwa ni baada ya mwaka wa ukombozi wa Makka

Muslim amepokea ndani ya *Sahih* yake toka kwa Abu Said kwamba amesema: “Tulikuwa tukisafiri na Mtume mwezi wa Ramadhani wala hamkosoi mwenye kufunga kwa Saumu yake wala mwenye kufungua kwa kufungua kwake.” **44**

Ametoa tena toka kwa Anas kuhusu Saumu ya Ramadhani safarini, amesema: “Tulisafiri na Mtume ndani ya Ramadhani na wala mwenye Saumu hakumkosoa aliyefungua wala aliyefungua

41. Sahih Muslim: 3/143, mlango wa ruhusa ya Saumu

42. Sahih Muslimu: 3/143

43.Al-Mahaliy: 6/247

44. Sahih Muslimu: 3/143, mlango wa ruhusa ya Saumu

hakumkosoa mwenye Saumu.” **45.**

Anajibiwa kuwa: Mtume alisafiri ndani ya mwezi wa Ramadhani mara moja katika vita vya Badr na mara nyingine ndani ya mwaka wa ukombozi. Hivyo nina imani hadithi hizi mbili zinahusu safari yake ndani ya Ramadhani katika vita vya Badri. Kinyume na hivyo haiwezekani kwani yeye amewapinga waliyomukhalifu na kufunga ndani ya Ramadhani mwaka wa ukombozi na akawa kawaita ni waasi.

Na hadithi hizi mbili ni shahidi kuwa ruhusa ya hiyari inayoonekana hapo ilikuwa kabla ya mwaka wa ukombozi wala si ndani ya mwaka wa ukombozi na wala si baada.

c) Ambazo njia ya upokezi wake ni dhaifu hivyo zenyewe si hoja.

Kuna riwaya dhaifu ambazo si hoja, hivyo hapa tutatoa mifano miwili tu:

Iliyopokewa kwa kuvushwa toka kwa Al-Atwarifu bin Haruna: Hakika watu wawili walisafiri mmoja wao kafunga na mwingine kafungua. Wakamwambia hilo Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema: Wote wawili mmepatia. **46**

Iliyopokewa kwa kuvushwa toka kwa Abu Iyadhi: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu aliamrisha inadiwe katikati ya watu kuwa mwenye kutaka kufunga afunge na mwenye kutaka kufungua afungue. **47**

---

45. Sahih Muslimu: 3/143, mlango wa ruhusa ya Saumu

46. Al-Mahaliy: 6/247

47. Al-Mahaliy: 6/247

Riwaya za kuvushwa si hoja. **48**

Riwaya aliyoipokea Ibnu Hazmi toka kwa Aisha **49** kuwa yeye Aisha alikuwa akifunga safarini na akitimiza sala, hali hiyo ni ijtihadi yake binafsi isiyofaa kuwa hoja, iwapo alifunga ndani ya mwezi wa Ramadhani baada ya mwaka wa ukombozi.

Matokeo ya mazungumzo ni kuwa riwaya hizi zipo zisizobainisha wazi kuwa Saumu ilikuwa ni ya Ramadhani. Au zimetamka wazi kuwa ni ya Ramadhani lakini hazijaweka wazi kuwa ni baada ya mwaka wa ukombozi wa Makka. Na nyingine njia za upokezi wake ni dhaifu hivyo hazitumiki kama hoja.

Na hata kama tukijalia kuwa riwaya hizi zinaonyesha ruhusa ya hiyari bado zitagongana na zile zinazotamka wazi kuwa kufungua ni lazima hivyo italazimu vigezo vya ziada vichukue nafasi.

Na kigezo cha kwanza ni kuafikiana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na ni wazi kuwa kundi la kwanza ndilo linaloafikiana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na Kitabu kimeonyesha wazi kuwa kufungua ni lazima.

Na mwisho wa dua yetu ni kumshukuru Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu wote.

Imetafsiriwa na:
Hemedi Lubumba Selemani (Lipumba)
Imehaririwa na Abdallah Mohamed

48. Al-Mahaliy: 6/247
49. Al-Mahaliy: 6/247

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na kumi na nane
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi

25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Maulidi.
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza swala safarini
51. Uadilifu wa Maswahaba

BACK COVER

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake, hivyo Mwenyezi Mungu akasema: "Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema Yangu na nimewapendeleeni Uislamu uwe dini yenu." (5:3).

Isipokuwa kuna masuala madogo madogo ambayo wanazuoni wa sheria wamehitilafiana kwa sababu ya kutofautiana kwao kuhusu riwaya ambazo zimenasibishwa kwa Mtume. Jambo ambalo limesababisha kutofautiana kuhusu masuala madodo madogo ya sheria.

Kwa kuwa ukweli hutokana na utafiti basi hakika katika mtiririko wa masomo haya mwandishi amejaribu kuliweka swala hili juu ya meza ya utafiti, kwani huenda ikawa ndio njia ya kuunganisha mtazamo na kusogeza hatua katika uwanja huu. Kwani tofauti iliyopo si katika asili na misingi ya dini hata isababishe kuwa na uadui na chuki, bali tofauti iliyopo ni kuhusu riwaya zilizonasibishwa na Mtume, nalo ni jambo dogo ukilinganisha na mambo mengi ambayo tunaafikiana kati ya madhehebu za Kiislamu. Na mwongozo wetu katika njia hii ni kauli ya Mwenyezi Mungu:
“Na shikamaneni katika kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, mlipokuwa maadui na akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema Zake mkawa ndugu." (3:103)

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Al-Itrah Foundation
P.O. Box 19701,
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu/Fax: +255 22 2127555
Email: alitrah@raha.com